



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU CHAGUZI NDOGO KATIKA JIMBO LA
BUHIGWE NA KATA KUMI NA NANE

Dar es Salaam, 9 Aprili, 2021


Kiti cha Mbunge wa Jimbo la Buhigwe, mkoani Kigoma kiko wazi kufuatia aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 30 Machi, 2021 na hivyo kukoma kuwa Mbunge kwa mujibu wa ibara ya 71(1)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katika hali hiyo, Kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinamtaka Spika atamtaarifu Mwenyekiti wa Tume kwa maandishi juu ya kuwepo kwa nafasi wazi ya kiti cha Mbunge. Tayari, Tume imekwishapokea taarifa hiyo kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Tume imepokea barua kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akiitarifu kuhusu kuwepo wa nafasi wazi za udiwani katika kata kumi na nane (18) Tanzania Bara.

Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na Kifungu cha 13(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume imeandaa chaguzi ndogo ili kujaza nafasi ya Mbunge iliyo wazi katika Jimbo la Buhigwe na nafasi wazi za udiwani katika kata kumi na nane (18) za Tanzania Bara. Ratiba ya Uchaguzi wa Mbunge na Madiwani katika kata 18 ni kama ifuatavyo:-

Na.	Tukio	Tarehe
1.	Wagombea kuchukua fomu za Uteuzi	24 - 30 Aprili, 2021
2.	Uteuzi wa Wagombea	30 Aprili, 2021
3.	Kampeni za Uchaguzi	01 hadi 15 Mei, 2021
4.	Siku ya Kupiga Kura	16 Mei, 2021

Imetolewa na:



Dkt. Wilson Mahera Charles

Mkurugenzi wa Uchaguzi

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

ORODHA YA NAFASI WAZI ZA MADIWANI, 2021

NA	MKOA	HALMASHAURI	NA	KATA
1	GEITA	GEITA DC	1.	BUGALAMA
2	IRINGA	KILOLO DC	2.	KISING'A
3	SHINYANGA	MSALALA DC	3.	JANA
4	PWANI	KIBAHA DC	4.	KIKONGO
5	GEITA	CHATO DC	5.	BUZIKU
6	MTWARA	TANDAHIMBA DC	6.	MIUTA
7	TABORA	NZEGA DC	7.	IGUSULE
		IGUNGA DC	8.	IGUNGA
		UYUI DC	9.	MMALE
8	RUVUMA	TUNDURU DC	10.	LIGOMA
9	ARUSHA	MONDULI DC	11.	ENGUTOTO
10	MBEYA	MBEYA DC	12.	IWIJI
11	TANGA	BUMBULI DC	13.	KISIWANI
12	NJOMBE	NJOMBE DC	14.	MATEMBWE
13	DODOMA	KONGWA DC	15.	SAGARA
14	KILIMANJARO	SAME DC	16.	MHEZI
15	KIGOMA	KASULU DC	17.	KAGERA NKANDA
			18.	NYAKITONTO